

GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXX Nam. 6905 **14 Aprili, 2021** **Bei Shs. 2,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

ALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na kuweka masharti bora ndani yake 273

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2021

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 5 Mei, 2021 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza, na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
14 Aprili, 2021

(Mhandisi Zena Ahmed Said)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na
Katibu Mkuu Kiongozi

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa

SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, 2021 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali.

2. Sheria zilizotajwa katika sehemu mbalimbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA MISITU NAM. 10 YA 1996

Kusomwa.

3. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996, ambapo katika sehemu hii itajuilikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 35.

4. Kifungu cha 35 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

SEHEMU YA TATU
MAREKEBISHO YA SHERIA YA UVUVI NAM. 7 YA 2010

Kusomwa.

5. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uvuvi Nam.7 ya 2010, ambapo katika sehemu hii itajuilikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

6. Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza ufafanuzi wa maneno yafuatayo kwa mpangilio wake wa kiherufi:

“Ufugaji wa viumbe maji” maana yake ni kitendo cha kulea au kukuza samaki au mazao ya baharini katika mazingira ya maji”;

“Diko” maana yake ni eneo la fukwe katika kijiji ambalo kwa kawaida hutumiwa na wavuvi kushushia samaki au kuegesha vyombo vya uvuvi baada ya kurejea kutoka katika shughuli zao za uvuvi vilevile hulitumia eneo hilo kwa matengenezo ya vyombo vya uvuvi na kufanya shughuli za utafiti zikiwemo ukusanyaji wa taarifa pamoja na shughuli nyengine zilizoidhinishwa na kamati za wavuvi;

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11A.

7. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 11A mara baada ya kifungu cha 11 kama ifuatavyo:

Uanzishwaji wa diko.

"11A. Kunaanzishwa diko linalojulikana kama diko katika kijiji cha mwambao ambalo liko pembezoni mwa fukwe ndani ya Zanzibar ambalo litaainishwa na Idara kwa kushirikiana na Taasisi husika za Serikali na litamilikiwa na Wizara".

SEHEMU YA NNE
MAREKEBISHO YA SHERIA YA ELIMU NAM. 6 YA 1982

Kusomwa.

8. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982, ambapo katika sehemu hii itajuilikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 17.

9. Kifungu cha 17 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

SEHEMU YA TANO
MAREKEBISHO YA SHERIA YA OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU NAM. 10 YA 2018

Kusomwa

10. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya 2018, ambapo katika sehemu hii itajulikana kama Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

11. Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka upya badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Ripoti ya skuli iliyokaguliwa itawasilishwa skuli na kwa Katibu Mkuu wa Wizara".

SEHEMU YA SITA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA NAM. 11 YA 2012

Kusomwa.

12. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira Nam. 11 ya 2012, ambapo katika sehemu hii itajuilikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

13. Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Majengo au maeneo au sehemu yoyote ya majengo au maeneo hayatokaliwa mpaka kibali cha afya kitakapotolewa na Mkaguzi".

Kuongezwa kifungu kipya cha 51A.

14. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 51A mara baada ya kifungu cha 51 kama ifuatavyo:

Uvunjaji wa majengo yasiyofaa.

"51A.-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa kushauriana na taasisi husika na baada ya kupata amri ya mahakama, kuvunja jengo lolote au sehemu ya jengo ambayo kwa maoni yake:

(i) imechakaa;

(ii) ina kasoro za kiujenzi;

(iii) imejengwa katika eneo la umma, eneo la wazi, njia au katika hifadhi yoyote ya barabara; au

(iv) ipo katika hali ambayo kwa kufanyiwa matengenezo au marekebisho halitoweza kuondosha usumbufu.

(2) Mkurugenzi analazimika, kabla ya kufanya ubomoaji chini ya kifungu hiki, kumtumia indhari ya siku kumi na nne mmiliki wa jengo au sehemu ya jengo ili ahame kabla ya siku iliyotajwa katika indhari hiyo.

(3) Endapo mmiliki ameshindwa kufuata maelekezo yaliyomo katika indhari chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania na atatakiwa kulipa gharama za ubomoaji.”

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 58.

15. Kifungu cha 58 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 58 kama ifuatavyo:

Taarifa ya maradhi ya kuambukiza.

“58.-(1) Endapo mmiliki au mtu mwenye dhamana ya eneo ambalo linatumika kwa ajili ya makaazi ya binaadamu ana maradhi ya kuambukiza au dalili za maradhi ambayo yanaweza kuleta mashaka kwamba ni maradhi ya kuambukiza, masharti yafuatayo yatafuatwa:

(a) Daktari anaeshiriki au aliyeitwa kumtembelea mgonjwa, atakapotambua kuwa mgonjwa anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza yanayodhaniwa kuwa amepata maambukizi, atapeleka taarifa kwa Afisa afya wa Wilaya inayoelezea jina na jinsia ya mgonjwa, hali ya eneo, vyanzo na sababu ya maradhi ambayo, kwa mawazo ya daktari huyo, mgonjwa huyo anasumbuliwa au anadhaniwa kuwa anasumbuliwa;

(b) Mgonjwa yeyote au jamaa wa mgonjwa ambaye amefanyiwa uchunguzi au anadhaniwa kupata maradhi ya kuambukiza atajuilishwa na daktari na atalazimishwa kufuata maelekezo aliyopewa na hatua zilizochukuliwa na Daktari; na

(c) Mtumiaji au mmiliki wa eneo, mara atakapojuwa kuwa mgonjwa anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza au anadhaniwa kuwa anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza, atatoa taarifa inayohusiana na maradhi hayo kwa mkuu wa kituo cha afya kilichokaribu na eneo ambalo mtu huyo anaishi ambaye atamjulisha Afisa afya wa Wilaya.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, meli au chombo chochote, wakati kipo katika bandari ya Zanzibar, kitachukuliwa kuwa ni nyumba na nahodha, mmiliki au mdhamini wa meli au chombo hicho atachukuliwa kuwa ni mkuu wa nyumba hiyo au mmiliki au anayeishi katika eneo hilo.

(3) Mtu anayetakiwa chini ya kifungu hiki kutoa taarifa au cheti akashindwa kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hitiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tano au kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote faini na kifungu.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, bandari inajumuisha bandari yeyote ya Zanzibar aidha iwe rasmi au isiyokuwa rasmi.

SEHEMU YA SABA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA NAM. 7 YA 2014

Kusomwa.

16. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya 2014 ambapo katika sehemu hii itajuilikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

17. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta ufafanuzi wa maneno "kilimo", "ufugaji wa viumbe maji", "mazao ya baharini" na "diko".

Kufutwa kwa kifungu cha 12.

18. Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 25.

19. Kifungu cha 25 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta aya (e).

Marekebisho ya kifungu cha 26.

20. Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya (i), (j) na (n) katika kifungu kidogo (1);

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2); na

(c) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (2).

Kufutwa kwa vifungu vya 26A, 26B, 26C, 39A, 86B na 86C .

21. Vifungu vya 26A, 26B, 26C, 39A, 86B na 86C vya Sheria Mama vinafutwa.

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 93A.

22. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 93A mara baada ya kifungu cha 93 kama ifuatavyo:

Miongozo.

"93A Waziri anaweza kuweka viwango vya kuandaa miongozo itakayotungwa na Mabaraza katika utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii."

Kufutwa kwa Jadweli la Kwanza.

23. Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linafutwa.

Kufutwa na Kuandikwa upya kwa Jadweli la Tatu.

24. Jadweli la Tatu la Sheria Mama linafutwa na kuwekwa badala yake Jadweli Jipya la Tatu kama ifuatavyo:

JADWELI LA TATU

KIAPO AU TAMKO LA UKWELI
(Chini ya kifungu cha 29)

Mimi, ……..., nimechaguliwa/ nimeteuliwa kuwa Diwani, naapa kwamba nitaitumikia ofisi yangu na nitakua muaminifu katika kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Sheria zilizowekwa, ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.

Kikao cha Pamoja kilichoitishwa …….. katika ukumbi wa Baraza la Jiji/ Baraza la Manispaa/Baraza la Mji/ Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya …….

……..
Saini

Kimeapiwa mbele yangu…… Hakimu wa Mkoa leo…….Mwezi……., 20…….

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kupendekeza marekebisho ya Sheria mbali mbali kama inavyoelezwa hapa chini. Marekebisho yaliyopendekezwa ni kwa ajili ya kurejesha majukumu ya kiutendaji kutoka katika Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu katika wizara husika kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mswada huu umegawika katika sehemu saba:

Sehemu ya Kwanza: Sehemu hii inaelezea masharti ya awali yanayojumuisha Jina fupi, na kuanza kutumika na Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Sehemu ya Pili: Sehemu hii inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996. Katika sehemu hii, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 35 kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

Sehemu ya Tatu: Sehemu hii inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya 2010. Katika sehemu hii inapendekezwa kufanya marekebisho ya kifungu cha 3 kwa kuongeza ufafanuzi wa maneno "kilimo", ufugaji wa viumbe maji", "mazao ya baharini" na diko" kwa mpangilio wake wa kiherufi vile vile inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11(A) mara baada ya kifungu cha 11.

Sehemu ya Nne: Sehemu hii inaelezea marekebisho ya Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982. Katika sehemu hii inapendekezwa kufanya marekebisho ya kifungu cha 17 kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

Sehemu ya Tano: Sehemu hii inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya 2018 na inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 8 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2).

Sehemu ya Sita: Sehemu hii inaelezea marekebisho ya Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira Nam. 11 ya 2012. Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 30 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1). Sehemu hii pia imeongeza kifungu kipya cha 51A mara baada ya kifungu cha 51 na kufuta na kuandikwa upya kifungu cha 58.

Sehemu ya Saba: Sehemu hii inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam. 7 ya 2014. Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 2 kwa kufuta ufafanuzi wa maneno "kilimo", "ufugaji wa viumbe maji", "mazao ya baharini" na "diko". Sehemu hii pia inafuta kifungu cha 12 na inafanya marekebisho ya kifungu cha 26 katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta aya ya (i), (j) na (n) pamoja na kufuta aya (e) katika kifungu cha 25(1) na kufuta kifungu kidogo cha (2) na kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (2). Sehemu hii pia inapendekezwa kufutwa kwa kifungu cha 26A, 26B, 26C, 39A, 86B, 86C, na pia inaongeza kifungu kipya cha 93A mara baada

ya kifungu cha 93 ambacho kinahusiana na nafasi ya Waziri katika uandaaji wa miongozo. Sehemu hii pia imefuta Jadweli la Kwanza na kufutwa na kuandikwa upya kwa Jadweli la Tatu.

ZANZIBAR
14 Aprili, 2021

DKT. MWINYI TALIB HAJI
MWANASHERIA MKUU
ZANZIBAR

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR - 2021